TANGAZO LA SERIKALI NA. 924 la tarehe 22/12/2023

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya Kifungu cha 153(1))*

SHERIA NDOGO YA USAFI WA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA YA MWAKA 2023

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ya Mwaka 2023.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Ngara.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote atakayeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chakula" maana yake ni kitu chochote kinacholiwa au kunywewa na binadamu isipokuwa dawa;

"chanzo cha maji" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Ngara;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"kizimba cha taka" maana yake ni kizimba cha taka au chombo maalum kilichowekwa na Halmashauri kwa ajili ya jamii kuhifadhia taka ngumu kabla ya kusafirishwa hadi kwenye jalala kuu lililoidhinishwa;

"mkazi" maana yake ni mtu yeyote ambaye kwa kawaida anaishi kwenye eneo lililoko chini ya mamlaka ya Halmashauri na ambaye ama ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri;

"maji taka" maana yake ni ile iliyoanishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"taka" maana yake ni ile iliyoanishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura ya 191

"taka ngumu" Maana yake ni ile iliyoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura ya 331

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, kampuni au shirika ambalo limeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi yoyote chini ya Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri.

Wajibu wa kufanya usafi wa mazingira

4.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi anayemiliki eneo la nyumba, kiwanja au biashara kuhakikisha kwamba-

(a) mazingira yanayozunguka eneo lake yanakuwa safi wakati wote;

(b) taka zote zinakusanywa na kufukiwa au kuondolewa kwa njia itakayoelekezwa na Halmashauri;

(c) anachimba shimo la kutupia taka litakalokuwa na urefu usiopungua kimo cha futi tatu na upana usiopungua futi mbili;

(d) anajenga choo imara cha kudumu kilichojengwa kwa matofali na kuezekwa kwa bati, tembe, majani, vigae chenye mlango unaofunga na kufunguka na kuhakikisha kwamba choo kinatumika wakati wote na kuwe na chombo cha

maji tiririka na sabuni ya kunawa mikono;

(e) eneo lake halina mazalia ya mbu, panya na wadudu wengine hatarishi;

(f) anaweka wavu maalumu kwenye gari lake ili kuzuia kumwagika kwa mchanga, taka au mbolea katika barabara au eneo lolote katika Halmashauri;

(g) anaweka chombo cha kuhifadhia taka ndani ya gari la abiria.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya aya ndogo ya (1) atakuwa ametenda kosa.

Uhifadhi wa maji taka

5.-(1) Kila mmiliki wa nyumba, kiwanda au eneo la biashara anatakiwa-

(a) kuhakikisha kuwa analo karo la kuhifadhi maji taka;

(b) kunyonya maji taka pale karo linapojaa; na

(c) kutotiririsha au kutoelekeza maji kutoka vyooni, bafuni, karoni au viwandani kwenda barabarani, uchochoroni, mtoni, kwenye vyanzo vya maji, maeneo ya wazi, kwenye mfereji wa maji ya mvua au sehemu yoyote isiyotengwa kuhifadhia maji taka.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya aya ndogo ya (1) atakuwa ametenda kosa.

Utengenezaji na uuzaji wa vyakula

6. Mtu yeyote anayetengeneza matunda, kuchoma, kupika, kuchemsha au kuuza chakula cha aina yoyote katika eneo la Halmashauri atatakiwa-

(a) kuzingatia masharti ya Sheria Ndogo hii; na

(b) kuwa na kibali kutoka kwa afisa afya wa Halmashauri.

Upimaji wa afya

7. Itakuwa ni wajibu wa kila mhudumu wa hoteli, migahawa, baa, nyumba za kulala wageni, bucha, waoka mikate, au watu wanaoshughulika na kuuza vyakula

vilivyopikwa kuhakikisha kwamba wanapima afya zao kila baada ya miezi sita.

Uwezo wa afisa mwidhiniwa

8.- (1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo kuingia katika eneo lolote ndani ya Halmashauri wakati wa muda wa kazi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

(2) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kushauri au kuelekeza watu au mtu kutokuishi katika jengo ambalo linahatarisha afya au maisha ya watu na viumbe hai.

Vifaa vya kuhifadhi taka ngumu

9.-(1) Kila mmliki wa jengo la makazi au mpangaji wa jengo la makazi au mtu yeyote anayefanya biashara katika eneo lolote au chombo cha usafiri ndani ya Halmashauri atatakiwa kuwa na chombo cha kuhifadhia taka chenye mfuniko na atawajibika kukusanya taka hizo kwenye vizimba vya kuzolea taka katika maeneo yaliyoainishwa.

(2) Kila mmiliki wa jengo au mpangaji wa nyumba iliyoko katika ukanda wa kijani, katika maeneo ambayo hayajapimwa atalazimika kuwa na shimo kubwa la kukusanyia taka ngumu katika eneo lake.

Ada ya uzoaji taka

10.-(1) Halmashauri itawajibika kukusanya taka ngumu kutoka katika vizimba vya taka vilivyoainishwa katika kila kata, na wazalishaji taka watalipia ada au ushuru wa ukusanyaji wa taka kama ilivyooneshwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

Ukusanyaji taka ngumu

11.- (1) Hairuhusiwi kuweka uchafu wenye asili ya maji maji kwenye pipa la taka au kitu chochote kinachoweza kulipuka na kusababisha madhara.

(2) Taka ngumu zote zitakazokusanywa kwenye mapipa ya taka zitabaki kuwa mali ya mkazi au mmliki wa eneo lile mpaka zitakapokuwa zimefikishwa kwenye kizimba cha taka au zitakapokuwa zimetolewa na wakala

kutoka katika eneo lake.

(3) Hairuhusiwi mtu yeyote kuchoma au kufukia taka ngumu bila kibali cha Halmashauri.

Eneo la kutupa taka

12.- (1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa-

(a) kutenga eneo maalum kwa ajili ya kutupia taka;
(b) kuweka vyombo maalum vya kutunzia taka katika maeneo ya Halmashauri; na
(c) kutoa huduma ya uzoaji taka kwa malipo kutoka kwa wazalishaji wa taka hadi kwenye dampo.

(2) Hairuhusiwi kwa mtu yeyote kuweka au kutupa taka, mchanga au uchafu wowote utakaoleta chukizo na uharibifu wa mazingira

Siku ya usafi

13.- (1) Kila alhamisi ya wiki na jumamosi ya mwisho wa mwezi itakuwa ni siku maalamu ya kufanya usafi wa mazingira katika maeneo ya makazi na umma.

(2) kila mkazi katika kijiji na kitongoji anapaswa kushiriki kufanya usafi wa mazingira kwa siku iliyopangwa na Halmashauri katika maeneo yao na maeneo ya umma.

(3) Kila mtu atahakikisha eneo la makazi yake na vichochoro vilivyomzunguka, eneo analofanyia biashara, eneo la wazi lililokaribu naye kwa umbali wa mita kumi na eneo la mazingira ya ofisi ni safi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(4) Halmashuri itaelekeza eneo fulani kufanyiwa usafi na kikundi, makundi au taasisi yotote iliyoko katika eneo la Halmshauri.

Vikundi vya kufanya usafi

14. Halmashauri itahamasisha uundaji wa vikundi jamii na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira katika mitaa baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

Wajibu wa wamiliki wa magari

15. Wamiliki wote wa magari yanayovuka mipaka watahakikisha kuwa-

(a) wanakagua magari yao mara kwa mara ili yanapopita ndani ya Halmashauri yawe katika hali njema;
(b) wanafunga mabomba imara ya kutolea moshi na hewa chafu ili yasipitishe hewa chafu itakayoharibu mazingira;
(c) magari yote yabebayo vifaa vya ujenzi au taka zitokanazo na mabaki ya ujenzi yanafunikwa;
(d) kutotupa taka ovyo muda wote wanapokuwa ndani ya Halmashauri; na
(e) wanaegesha magari sehemu maalum iliyotengwa na Halmashauri.

Marufuku

16. Ni marufuku kwa mtu yeyote:
(a) kuendesha biashara ya upulizaji dawa au biashara ya kuua wadudu au wanyama waharibifu katika nyumba yoyote au mahali popote bila cheti cha taaluma kinachotambuliwa na Serikali na leseni kutoka Halmashauri;
(b) mfanyabiashara kupanga bidhaa nje ya jengo lake la biashara, barabarani, vichochoroni au katika eneo lolote ambalo halikuidhinishwa kwa ajili ya shughuli hiyo;
(c) mfugaji kuruhusu mifugo kuzurura ovyo mitaani au barabarani;
(d) kutupa taka za aina yoyote barabarani au eneo lolote la wazi, kwenye vichochoro au kwenye chanzo chochote cha maji au katika eneo lolote ambalo halikutengwa kwa ajili ya shughuli hiyo;
(e) aliye ndani ya gari kudondosha taka ngumu nje ya gari likiwa ndani au nje ya kituo cha magari na sehemu yoyote ile ambapo gari hilo linapita;
(f) kuanzisha shughuli za kiwanda au mradi wowote unaoweza kuathiri mazingira bila kufanya utafiti wa mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;
(g) kuzuia maji kupitia njia yake ya asili kwa

kujenga au kulima au kuweka kitu chochote kwenye maji kitakachoingilia mtiririko wa asili wa maji katika chanzo cha maji;

(h) kuweka kitu chochote kwenye maji taka ambacho kinaweza kuathiri mtu yeyote au kuharibu mfumo wa tiba ya maji taka au kinachoweza kusababisha kuzuia mtiririko wa maji taka;

(i) kulima kilimo cha matuta yanayosababisha maji kutuama ndani ya eneo la katikati ya mji;

(j) kuchimba mchanga, kokoto au mawe katika vyanzo vya maji, mito barabarani;

(k) kujenga kisima cha maji bila idhini ya maandishi ya Halmashauri;

(l) kuchafua, kuoga, kufulia au kuvuruga maji yanayotumika kwa ajili ya matumizi ya binadamu au wanyama;

(m) kuuza mchanga, kokoto na mawe kandokando mwa barabara;

(n) kukata mti uliokwisha pandwa au ulioota wenyewe bila kupata kibali cha Halmashauri ambacho kitatolewa kwa masharti maalum;

(o) kuegesha au kufanya matengenezo ya gari, pikipiki au baiskeli kwenye maeneo ya makazi, bakaa za barabara maeneo ya wazi;

(p) kufanya biashara ya pombe ya aina yoyote katika nyumba, au kwenye maeneo ya akiba za barabara, mitaani;

(q) kuuza matunda au bidhaa nyingine za vyakula barabarani au kuanzisha masoko au magenge ya kuuzia matunda, vyakula au biashara nyingine ndogo bila ruhusa ya Halmashauri;

(r) kuunganisha bomba la taka vimiminika katika mifereji ya maji ya mvua;

(s) kufungulia au kutiririsha maji ya choo au taka vimiminika katika mkondo asili wa maji ya mvua au barabara au mfereji wa barabara wa

maji ya mvua;

(t) kujisaidia haja ndogo au haja kubwa barabarani au mitaani au sehemu yoyote isiyokusudiwa kwa madhumuni hayo;

(u) kubomoa jengo lolote kwa njia yeyote ile bila kupata kibali cha Halmashauri;

(v) kuhakikisha mifugo haizururi ovyo, na kinyesi au uchafu wowote unaotokana na wanyama wafugwao unatupwa ovyo na kuleta kero kwa jamii;

(w) mzalishaji, mfanyabiashara au mchuuzi wa mazao au vitu vinavyoharibika kuingiza sokoni vitu hivyo vikiwa vimefungwa au kufunikwa kwa majani ya miti au aina yeyote ile ya sehemu ya mimea;

(x) kufanya mikusanyiko ya kidini, kiutamaduni au kijamii wakati wa milipuko ya magonjwa ya kuambukiza, isipokuwa kwa ruhusa maalum ya Halmashauri na usimamizi wa Afisa Afya; na

(y) kuchoma moto takataka za majumbani, makaratasi, majani, michongoma au takataka za aina yeyote katika maeneo ya makazi ya watu na kusababisha moshi kwa wakazi na kuchafua hewa kwa moshi na mazingira kwa ujumla.

Makosa

17. Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hii kwa mtu yeyote-

kujenga choo chini ya umbali wa mita sitini kutoka kisimani, bwawani, mtoni, au chanzo kingine cha maji yanayotumika, kwa matumizi ya binadamu;

kutoa kinyesi au kusababisha kinyesi, mkojo, maji machafu, yenye kinyesi kutoka kwenye choo chake au bafu lake au karo la kuoshea vyombo au nguo au kutoka kwenye bomba lolote linalochukua maji machafu na kuyatitirisha kwenye barabara, mitaa, au kwenye mifereji ya maji ya mvua, au mfereji wowote uliowazi;

(a) kutupa taka au kusababisha mtu mwingine atupe taka mahali popote pasiporuhusiwa na Halmashauri;
(b) kuuza chakula nje ya eneo ambalo halijasajiliwa kwa ajili ya shughuli hiyo;
(c) kuzika maiti katika eneo ambalo halikuainishwa kwa shughuli hiyo;
(d) kutolipa ada ya taka kwa miezi miwili mfululizo;
(e) kutembeza vyakula mitaani bila kibali cha Halmashauri;
(f) kuchezesha michezo au kuonyesha michezo au burudani katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri;
(g) kuegesha gari bovu na kuliacha kando ya barabara au kichochoro au eneo la wazi ambalo halijaidhinishwa kwa shughuli za gereji na kuliacha zaidi ya siku moja;
(h) kulima ndani ya vyanzo vya maji;
(i) kutokuwa na pipa la taka lenye mfuniko katika eneo la biashara;
(j) kutokuwa na choo au kukutwa na choo kibovu au kilichojaa;
(k) kukutwa na shimo la maji taka lililojaa au ambalo halina mfuniko;
(l) kuziba kichochoro; na
(m) kutokuwa na chombo maalum cha kukusanyia taka ndani ya gari la abiria na mizigo.

Adhabu

18. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na endapo akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Shilingi elfu hamsini na isiyozidi Shilingi laki tatu au kutumikia kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

19. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi cha Shilingi elfu hamsini iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

JEDWALI LA KWANZA

(*Limetengenezwa chini ya aya ya (10)*)

A: ADA ZA UZOAJI TAKA

| Na | Aina ya biashara | Viwango |
|---|---|---|
| 1 | Maduka ya madawa na pembejeo za kilimo na mifugo | 10,000/= Kwa mwezi |
| 2 | Duka dogo la rejareja | 5,000/= Kwa mwezi |
| 3 | Karakana za ufundi wa aina mbalimbali | 5,000/= Kwa mwezi |
| 4 | Baa/Duka la vinywaji baridi | 5,000/= Kwa mwezi |
| 5 | Nyumba ya kulala wageni. | 10,000/= Kwa mwezi |
| 6 | Saluni za nywele za kike na kiume | 5,000/= Kwa mwezi |
| 7 | Kituo cha kuuza mafuta | 30,000/= Kwa mwezi |
| 8 | Klabu cha kuuza pombe za asili | 5,000/= Kwa mwezi |
| 9 | Usafi wa soko kwa kila mfanyabiashara aliyeleta bidhaa. | 200/=Kwa siku |
| 10 | Nyama ya kuchoma | 5,000/= Kwa mwezi |
| 11 | Zahanati | 10,000/= Kwa mwezi |
| 12 | Washona viatu na nguo | 5,000/= Kwa mwezi |
| 13 | Shughuli nyingine yeyote ambayo haijatajwa hapa | 5,000/= Kwa mwezi |
| 14 | Maegesho ya magari mapya yanayosafirishwa kwenda nje ya mipaka ya Tanzania pamoja na maegesho ya kuuzia magari mapya | 30,000/=kwa mwezi |
| 15 | Mgahawa mdogo | 5,000/= Kwa mwezi |
| 16 | Mgahawa mkubwa | 10,000/= Kwa mwezi |
| 17 | Zahanati (taka zisizohatari) | 10,000/= kwa mwezi |

*Tangazo La Serikali Na. 924 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 18 | Kituo cha afya (taka zisizohatari) | 10,000/= kwa mwezi |
| 19 | Hospitali ya Rufaa (taka zisizohatari) | 50,000/= kwa mwezi |
| 20 | Hospitali ya Wilaya/Mkoa (taka zisizohatari) | 50,000/= kwa mwezi |
| 21 | Kiwanda cha mbao | 30,000/= kwa mwezi |
| 22 | Fundi Seremala (mdogo) | 5,000/= Kwa mwezi |
| 23 | Fundi chuma | 15,000/= kwa mwezi |
| 24 | Karakana nyinginezo (magari na pikipiki) | 20,000/= kwa mwezi |
| 25 | Kiwanda kidogo | 50,000/= kwa mwezi |
| 26 | Kiwanda kikubwa | 200,000/= kwa mwezi |
| 27 | Duka la jumla | 10,000/= kwa mwezi |
| 28 | Duka la rejareja/huduma | 5,000/= Kwa mwezi |
| 29 | Shule ya Msingi ya Bweni | 15,000/= kwa mwezi |
| 30 | Shule ya Sekondari ya Bweni | 30,000/= kwa mwezi |
| 31 | Kituo cha kulelea watoto | 5,000/= Kwa mwezi |
| 32 | Kituo cha kutunzia watu wenye mahitaji maalum | Bure |
| 33 | Duka dogo la chakula | 5,000/= Kwa mwezi |
| 34 | Duka kubwa la chakula | 30,000/= kwa mwezi |
| 35 | Baa kubwa | 20,000/= kwa mwezi |
| 46 | Klabu ya usiku | 40,000/= kwa mwezi |
| 37 | Kumbi za Sherehe | 25,000/= kwa mwezi |
| 38 | Duka la kuuza nyama na samaki | 5,000/= Kwa mwezi |
| 39 | Nyama choma/chipsi inayojitegemea | 5,000/= Kwa mwezi |
| 30 | Duka la Dawa (Jumla na Rejareja) | 25,000/= kwa mwezi |
| 41 | Duka la Dawa (DLDM - Rejareja) | 10,000/= kwa mwezi |
| 42 | Kiwanda kidogo | 50,000/= kwa mwezi |
| 43 | Dobi mdogo | 5,000/= Kwa mwezi |
| 44 | Dobi mkubwa | 10,000/= kwa mwezi |
| 45 | Fundi wa vifaa vya umeme | 5,000/= Kwa mwezi |
| 46 | Fundi kushona(ofisi) kwa kila cherehani | 5,000/= Kwa mwezi |
| 47 | Duka la kuuza spea | 10,000/= kwa mwezi |
| 48 | Stoo za kuhifadhia mizigo | 5,000/= Kwa mwezi |
| 49 | Ghala | 30,000/= kwa mwezi |
| 50 | Hoteli | 20,000/= kwa mwezi |
| 51 | Taasisi | 100,000/= kwa mwezi |
| 52 | Klabu ya pombe ya asili | 5,000/= Kwa mwezi |
| 53 | Dahalia | 10,000/= kwa mwezi |
| 54 | Kituo cha michezo | 10,000/= kwa mwezi |
| 55 | Uwanja wa michezo | 10,000/= kwa mwezi |
| 56 | Ofisi za wauza viatu na nguo za mitumba | 5,000/= Kwa mwezi |
| 57 | Stoo za mkaa | 5,000/= Kwa mwezi |
| 58 | Mama lishe/Baba lishe | 5,000/= Kwa mwezi |
| 59 | Duka la kuuza Magari | 30,000/= kwa mwezi |
| 60 | Sehemu za kuoshea vyombo vya usafiri | 30,000/= kwa mwezi |

B: ADA YA UNYONYAJI WA MAJI MACHAFU KWA KUTUMIA MAGARI YA HALMASHAURI

i. Maeneo ya biashara……………...………Shilingi. 300,000/= kwa kila safari moja.
ii. Maeneo ya makazi………………………Shilingi. 200,000/= kwa kila safari moja.
iii. Nje ya Halmashauri…………………….Shilingi. 500,000/= kwa kila safari moja.

C: ADA ZINAZOHUSIANA NA MIZIGO NA KUTUPA TAKA

1. Kutupa taka kwenye eneo lililotengwa na Halmashauri Shilingi. 5,000/= kwa safari moja
2. Kila gari litakaposhusha au kupakia mzigo litalipa kiasi cha Shilingi 10,000/=
3. Kufaulisha mizigo kwenye Maegesho ya Rusumo na Kabanga :
   i. Gari chini ya Tani 10 - Shilingi. 50,000/=
   ii. Gari chini ya Tani 25 - Shilingi. 75,000/=
   iii. Gari zaidi ya Tani 26 - Shilingi. 100,000/=

D:ADA KWA AJILI YA MAEGESHO YA KABANGA, BENACO NA KAHAZA

| AINA YA GARI | KIWANGO |
|---|---|
| Magari makubwa | Shilingi 3,000/= kwa siku |
| Magari madogo | Shilingi 3,000/= kwa siku |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 19)*

KUFIFILISHA KOSA

Mimi ………………………………. Nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya…………………………………..…ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara kwamba mnamo tarehe…………ya Mwezi…......... Mwaka …………….. nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya ………. ya Sheria Ndogo za Usafi wa Mazingira za Halmashauri ya Wilaya ya Ngara za Mwaka 2023.

*Tangazo La Serikali Na. 924 (Linaendelea)*

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, Niko tayari kulipa kiasi cha Shilingi…………… kwa ajili ya kufifilisha Kosa nililotendachini ya Sheria Ndogo ya Usafi wa Mazingira ninaodaiwapamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.

Leo tarehe………..ya Mwezi……………………Mwaka…………………..
Jina……………………………..…………….Saini……………………….
MBELE YA:
Jina…………………………………………….…..
Wadhifa……………………..…………………….…..
Saini…………………………………………………
Tarehe……………………………………………….

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya Ngara imegongwa kwenye sheria Ndogo hii kufutia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Ngara uliofanyika Tarehe 27 Mwezi Oktoba Mwaka 2021 na Kushudiwa na Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya :-

SOLOMON. O KIMILIKE
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Ngara*

WILBARD. J. BAMBARA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Ngara*

NAKUBALI,

Dodoma,
31 Oktoba, 2023

MOHAMED OMARI MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais,*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*